

Dhiki nchini

1. Dhiki imeshamiria, imeingia nchini
Wananchi wanalia, washangaa kulikoni?
Riziki kutafutia, popote ughaibuni
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
2. Baba na mama ugomvi, haukwishi majumbani
Vijana waota mvi, wakunjamana usoni
Barazani kwenye jamvi, hapakaliki jamani
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
3. Hodi imepiga dhiki, hata huko vijijini
Mijini hapakaliki, kote kote ni njaani
Bei hazikamatiki, uingiapo dukani
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
4. Imani imepungua, hata walio na dini
Usiombe kuugua, upate operesheni
Utadhani waungua, japokuwa u wodini
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
5. Viatu waviangaza, uwapo Msikitini
Siri waweza iuza, uungame Kanisani
Wazoa bila kusaza, viwachwavyo Tambikoni
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
6. Wenye nazo wanapeta, wajiona wa peponi
Wanasema wana data, ziwatoazo dhikini
Wanachanganya karata, wajiona wana wini
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
7. Yarabi tunakuomba, utuondoe njaani
Hatukucheza sindimba, tulipokuwa shambani
Tungalikuwa ni simba, tusingeacha majani
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
8. Na hao wawekezaji, hawaweki viwandani
Wawekezaji magwiji, watuingiza mijini
Kazi sio za wenyeji, kisa kwalifikesheni!
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
9. Yao macho yamezibwa, walio madarakani
Serikalini wakubwa, kesho wasema njooni
Hatuna japo ubwabwa, tutaonaje mbeleni?
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?
10. Kumi n'natimizia, ninaishia betini
Dhiki kuzungumzia, sijaleta ufitini
Msisite kujazia, muonapo walakini
Dhiki imekuwa dhiki, ni wapi tukimbilie?

***Msanif Shaaban
S.L.P 2180335
Dar es Salaam
Tanzania***